

imeendelea kuchangia uzalishaji wa ajira kwa

anasema Dk Tax.

Aidha, Dk. Tax ameahidi

inatengeneza maunzi laini maalum ilianza mwaka 2020 'software' zake yenyewe na inayoshughulikia usalama

ia kuanzishwa uwekezaji nchini.

TANZANIA DAIMA. UK 10.

Uvuvi kukuza uchumi wa buluu

VICTOR KAREGA

vkarega@tanzaniadaima.co.tz

UTEKELEZAJI wa mpango wa Sekta ya Uvuvi kwa miaka 15 utasaidia kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa hadi asilimia 10 kwa mwaka kutoka asilimia 1.8 ya sasa.

Akizungumzia kuhusu mpango huo kabambe unaotekelezwa kuanzia 2021/22 hadi 2036/37, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anasema ni muhimu katika

ukuajii wa sekta ya uvuvi na uchumi wa buluu.

Majaliwa, anasema Serikali ina nia ya dhati kuhakikisha kila mmoja ananufaika na sekta hiyo.

"Tunaendelea kupokea mapendekezo ya wadau ili tuweze kuboresha sekta hii, ubunifu wenu ni muhimu, wote tunataka tuzungumze lugha moja", Majaliwa anasema

Waziri Mkuu, anafanua kuwa mpango huu utasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza dhamira hiyo njema

ya Rais Samia Hassan.

Uwepo wa mipango katika sekta ya uvuvi utawezesha rasilimali hiyo kulindwa, kusimamiwa, kuendelezwa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu na hatimaye kuchangia kikamilifu katika kutoa ajira, kipato, chakula na lische kwa jamii ya Watanzania, kwa mujibu wa Waziri Mkuu.

Utekelezaji wa mpango huo utakuwa chachu ya kuendeleza kasi ya ukuaji wa sekta ya uvuvi na utasaidia kuongeza kiasi cha samaki na mazao

ya uvuvi yaliyochakatwa na kusafirishwa nje ya nchi kwa asilimia 30.

Pia, mpango huo utakuwa chachu ya kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya uvuvi kutoka tani 473,592 hadi kufikia tani 639,092, sawa na ongezeko la asilimia.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, anasema mpango huo utakuwa jumuishi na hautamuacha yeyote anayejishughulisha na sekta ya uvuvi.

Mwenyekiti wa Bodi ya

Wakurugenzi wa Shirika la Uvuvi Tanzania, Profesa Yunus Mgaya, anasema mpango huo utaleta maendeleo katika sekta ya uvuvi kwa kipindi cha miaka 15.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Tipo Nyabenyi, alisema wamefurahi kushirikishwa na serikali katika uandaaji wa mpango huo ambao wanaamini kwa kiasi kikubwa utaleta mchango katika kutatua changamoto mbalimbali za sekta hiyo.